



Kituo cha Utetezi cha Kitaifa, kilicho jijini Washington, D.C., ni Shirika Lisilo la Kiserikali linaloongoza katika fani ya sheria za utetezi. Tumekuwa tukifanya kazi kulinda na kuwapa mostisha watetezi kwa zaidi ya miaka 30.

Mtetezi ni nani?

Mtetezi ni mtu ambaye huripoti kuhusu rushwa, honga ya maafisa wa serikali, uhalifu dhidi ya wanyamapori au ukiukaji mwingine wa sheria kwa mamlaka husika, mara nyingi akihatarisha maisha yake binafsi kwa kuripoti. Kwa mujibu wa baadhi ya sheria, mashirika yasiyo ya kiserikali pia huzingatiwa kuwa "watetezi."

Watetezi ni Tegemeo Kubwa la kukabiliana na usafirishaji haramu wa wanyamapori!

Katika miaka ya hivi majuzi, uhalifu dhidi ya wanyamapori umeongezeka pakubwa, hivyo badi kutishia usalama na utulivu wa mataifa mengi.

Usafirishaji haramu wa wanyamapori ni sekta ya kimataifa ya thamani ya mabilioni ya dola, na visa vya kukamatwa na kushtakiwa kwa mashukiwa wake ni vichache mno.

Kuwahamasisha watetezi, wale walio na ujuzi wa kindani, kutasababisha mageusi makubwa katika juhudi za kugundua uhalifu, kuboresha uwezo wa kutii na kutekeleza sheria husika, na kugeuza tatizo la kutoweka kwa wanyamapori.

Tuzo za Watetezi

Watetezi wa kimataifa wamepokea zaidi ya dola milioni 30 kwa kutoa ripoti kuhusu rushwa ya maafisa wa kigeni chini ya sheria za tuzo za Marekani.

Serikali ya Marekani imelipa zaidi ya dola milioni 31.8 kwa watetezi wasio wa Kimarekani wanaoripoti kuhusu uchafuzi wa bahari kuu.

Mpango wa Watetezi wa Kimataifa wa Wanyamapori wa NWC hutumia vifungu vya utetezi katika sheria kama vile Sheria ya Lacey, Sheria ya Matendo ya Ufisadi wa Kigeni, na Sheria ya Madai ya Uongo ili kuwashawishi watetezi wa kisirisiri kutoa ripoti kuhusu usafirishaji haramu wa wanyamapori na uhalifu mwingine dhidi ya wanyamapori.



Serikali ya Marekani imelipa zaidi ya dola milioni 31.8 kwa watetezi wasio wa Kimarekani wanaoripoti kuhusu uchafuzi wa bahari kuu.

Mpango wa Watetezi wa Kimataifa wa Wanyamapori wa NWC ulishinda Tuzo Kuu la Shindano la Teknolojia ya Uhalifu Dhidi ya Wanyamapori la 2016, ambalo ni Mpango wa USAID kwa kushirikiana na Chama cha National Geographic, Taasisi ya Smithsonian na TRAFFIC. Mpango huu pia hupokea ruzuku kubwa kutoka Wakfu wa Wildcat.

Kutoa Ripoti za Ushahidi wa Uhalifu Dhidi ya Wanyamapori

Unaweza kuamua kuwa mtetezi wa uhalifu dhidi ya wanyamapori ikiwa umejua mwenyewe kuhusu uhalifu huo na una hati za kutoa uthibitisho kuhusu shughuli haramu. Kukusanya na kuandaa ushahidi kuhusu uhalifu dhidi ya wanyamapori ulioshuhudia ni jambo muhimu. Vyombo vya kutekeleza sheria zina uwezekano mkubwa wa kuchunguza ripoti wakati ikiwa zimeambatana na ushahidi wa kutosha:

- Picha
- Barua pepe
- Kadi ya Biashara
- Ripoti za Kisayansi
- Rekodi za Malipo
- Bajeti na Data ya Kifedha
- Ripoti za Ndani
- Vidokezo vya Mkutano
- Rekodi za Video na Sauti
- Matokeo ya Vipimo vya Kisayansi
- Njia za Usafiri na Mbinu za Usafirishaji
- Maelezo ya Akaunti ya Benki
- Ushahidi wa Rushwa na Uchapishaji Haramu wa Pesa

Watu walio na habari kuhusu ukiukaji wa sheria za ulinzi wa wanyamapori katika taifa LOLOTE wanashauriwa kutafuta ushauri wa kisheria kuhakikisha kuwa habari walizo nazo zimetunzwa kwa njia salama.

Tuzo na Ulinzi wa Watetezi

Kuna sheria za Marekani ambazo ni dhabiti na zinaweza kutumika kimataifa, ambazo zimebuniwa ili kupambana na uhalifu dhidi ya wanyamapori, na zenye vipengele mwafaka vya tuzo za watetezi.

Sheria hizi za tuzo huwasaidia watetezi duniani kote ambao hufichua matukio ya ukiukaji sheria muhimu za wanyamapori ambazo hulinda wanyama, samaki, mimea na viumbe vilivyo hatarini dhidi ya uvunaji, usafirishaji na uagizaji haramu nchini Marekani au na raia wa Marekani au makampuni yanayohusiana na nchi ya Marekani.

Mpango wa Watetezi wa Kimataifa wa Wanyamapori wa NWC hutoa mfumo salama na wa siri kabisa wa mtandaoni ambapo watu kutoka duniani kote hutoa ripoti kuhusu uhalifu dhidi ya wanyamapori, na kisha kuwaunganisha watetezi kwa mawakili ambao wanaweza kusaidia kuwasilisha ripoti zao kwa viongozi wa Marekani na kuomba kupewa tuzo chini ya sheria mwafaka za Marekani.

www.whistleblowers.org/wildlife

help@whistleblowers.org

